

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MALINYI



## TANGAZO LA ZABUNI YA UTOAJI HUDUMA MBALIMBALI KWA HALMASHAURI MWAKA WA FEDHA 2018/2019

TAREHE 25/07/2018

1. Halmashauri ya wilaya ya Malinyi imetenga fedha kutoka vyanzo vyake mbalimbali kwa ajili ya ununuzi wa huduma na vifaa na kazi mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Halmashauri imedhamiria kutumia sehemu ya fedha hizo kwa ajili kulipia huduma, kazi na vifaa mbalimbali kwa mwaka huu wa fedha kwa kazi ambazo zimeorodheshwa katika jedwali hapa chini. Halmashauri ya wilaya ya Malinyi inatarajia kuwachagua wazabuni ambao watafanya kazi hizo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kufanya kazi hizo za uuzaji vifaa, kazi, na huduma mbalimbali.
2. Uchaguzi wa wazabuni hao utafanywa kwa kufuata taratibu zilizoainishwa katika kanuni 119 ya sheria ya Manunuzi ya Umma na ni wazi kwa watu wote kama inavyoainishwa katika kanuni hizo.
3. Wombaji wanaotaka kuomba kazi hizo wanaweza kupata taarifa na kukagua kabrasha za zabuni katika **Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya wilaya ya Malinyi, Makao makuu ya wilaya, kijiji cha Makerere, ofisi ya Manunuzi, kuanzia saa 2.30 asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri, Jumatatu hadi Ijumaa** isipokuwa jumamosi na jumapili na siku za sikukuu za kitaifa..

NO	Namba ya zabuni	Jina la Zabuni
<b>BIDHAA (GOODS)</b>		
1.	LGA/176/2018/2019/G/01/Lot 01	Uuzaji wa vipuri vya magari, pikipiki na mitambo.
2.	LGA/176/2018/2019/G/01/Lot 02	Uuzaji wa Diesel, Petrol na Gesi.
3.	LGA/176/2018/2019/G/01/Lot 03	Uuzaji wa vifaa vya umeme
4.	LGA/176/2018/2019/G/01/Lot 04	Uuzaji wa vifaa vya ujenzi.
5.	LGA/176/2018/2019/G/01/Lot 05	Uuzaji wa samani za ofisi na majumbani.
<b>KAZI ZA UJENZI (MINOR WORKS)</b>		
6.	LGA/176/2018/2019/W/01/Lot 01	Ujenzi mdogo na marekebisho ya majengo.
<b>HUDUMA ZISIZO ZA KITAALAM (NON CONSULTANCY)</b>		
7.	LGA/176/2018/2019/NC/01/Lot 01	Huduma za upuliziaji viudadu katika majengo ya Halmashauri

8.	LGA/176/2018/2019/NC/01/Lot 02	Utoaji wa huduma ya kufanyia matengenezo mashine za ofisi, mfano Kompyuta, fax na photocopy.
9.	LGA/176/2018/2019/NC/01/Lot 03	Uchapaji nyaraka
10.	LGA/176/2018/2019/NC/01/Lot 04	Utoaji wa huduma ya kufanyia matengenezo mashine za Hospital.
11.	LGA/176/2018/2019/NC/01/Lot 05	Utoaji wa huduma ya kufanyia matengenezo ya magari ya Halmashauri
12.	LGA/176/2018/2019/NC/01/Lot 06	Huduma ya utoaji vyakula katika vikao na ugeni wa Halmashauri.
13.	LGA/176/2018/2019/NC/01 Lot 07	Utoaji wa huduma ya kufanya usafi na utunzaji wa bustani.

4. Kabrasha kamili la zabuni uombaji zabuni hizo likiwa katika lugha ya Kiingereza linaweza kununuliwa na mzabuni anaetaka kufanya kazi na Halmashauri, kwa kuandika barua ya maombi kwa anwani iliyopo katika paragrafu namba 4 hapo juu, ikiwa pamoja na ada ya uombaji zabuni ya kiasi cha shilingi 100,000.00 (LAKI MOJA) ambayo haitarudishwa malipo yakiwa ni Fedha taslimu.
5. Maombi yote yakiwa katika nakala halisi moja na nakala kivuli mbili zikiwa zimejazwa vizuri na kufungwa vizuri katika bahasha inatakiwa kutumwa kwa anwani:- **Katibu Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya wilaya ya Malinyi, S.L.P 18, Malinyi** kabla au tarehe 9 Agosti 2018 saa 4.30 asubuhi na kufuatiwa na ufunguzi wa wazi wa zabuni hizo kwa waombaji au wawakilishi watakao penda kuhudhuria ufunguzi huo utakaofanyika katika **ukumbi wa Halmashauri ya wilaya ya Malinyi.**
6. Zabuni zitakazo chelewa au zisizo kamili au zitakazotumwa kwa mtandao, zisizopokelewa na ambazo hazijasomwa wakati wa ufunguzi huo hazitakuabika na kufanyiwa tathmini za zabuni.

**Marcelin R. Ndimbwa**  
**Mkurugenzi Mtendaji Wilaya**  
**Halmashauri ya wilaya ya Malinyi**